

HEROES COMMUNITY ACADEMY (HCA)



TAARIFA NA MASHARTI YA UDAHILI WA WANAFUNZI

Elimu ya Awali / Maandalizi (Nursery)

Mwaka wa Masomo 2026/2027

Heroes Community Academy ni shule ya kisasa inayotoa elimu bora kwa viwango vya juu kwa kuunganisha taaluma, maadili mema, ubunifu na maendeleo ya mtoto kwa ujumla. Dhamira yetu ni kuwajengea watoto maarifa, stadi na maadili yatakayowawezesha kuwa viongozi, wabunifu na raia wenye uwezo wa kushindana kitaifa na kimataifa.

Kwa nini uchague Heroes Community Academy?

1. Shule ina mazingira salama, rafiki na vifaa vya kisasa vya kujifunzia.
2. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika ufundishaji na mawasiliano, pamoja na programu maalumu za kuimarisha Kiingereza kwa kila darasa.
3. Walimu wenye sifa na uzoefu kutoka ndani na nje ya Tanzania.
4. Mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA/ICT).
5. Fursa za msaada wa masomo kwa baadhi ya watoto wenye changamoto za kiuchumi kupitia wadau na wafadhili wa shule.
6. Michezo na shughuli za kukuza vipaji, ubunifu na kujiamini kwa wanafunzi.

Masharti ya kujiunga na masomo

1. Mwanafunzi anayeomba kujiunga na darasa la maandalizi anatakiwa awe na umri wa miaka minne (04).
2. Mwanafunzi anayehamia kutoka shule nyingine atafanyiwa usaili kama sehemu ya vigezo vya kukubaliwa kujiunga na shule.
3. Mwanafunzi anayehamia kutoka shule nyingine lazima awasilishe nyaraka zote muhimu kutoka shule aliyokuwa akisoma; bila nyaraka hizo, ombi lake la kujiunga halitakamilishwa.
4. Mzazi au mlezi anatakiwa kuwasilisha nakala za nyaraka zifuatazo:
 - (a) Cheti cha kuzaliwa.
 - (b) Cheti cha group la damu ya mtoto anaesajiliwa (blood group type).
 - (c) Picha moja ya ukubwa wa pasipoti iliyopigwa hivi karibuni.

Masharti ya malipo kwa Mwaka wa Masomo 2026/2027

Mzazi, mlezi au mdhamini anatakiwa kusoma na kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Mdhamini, mzazi au mlezi anawajibika kufanya malipo yote ya mtoto wake kwa mujibu wa makubaliano na utaratibu uliowekwa na shule.
2. Ada ya muhula husika inapaswa kulipwa kikamilifu kabla ya mwanafunzi kuanza masomo ya muhula huo (Muhula wa Kwanza au Muhula wa Pili).
3. Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo kwa muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026 na muhula wa pili ni 25/06/2027.
4. Mdhamini, mzazi au mlezi anaweza kulipa ada za mihula yote miwili kwa pamoja.
5. Mwanafunzi hatapewa kibali cha uhamisho endapo ana deni lolote la shule.
6. Endapo mwanafunzi atasitishwa masomo kwa sababu ya deni, deni hilo litaendelea kudaiwa hadi litakapolipwa kikamilifu.
7. Malipo yote yafanywe kupitia akaunti ya shule katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kwa kutumia Control Number, au kwa mhasibu wa shule badala yake malipo yasifanywe kwa njia nyingine yoyote.
8. Mzazi au mlezi anakubali kuwa masomo ya mtoto yanaweza kusimamishwa endapo masharti ya malipo yaliyotajwa hapo juu hayajatekelezwa ipasavyo.

Muhimu: Malipo yafanywe kwa njia zilizoidhinishwa na shule pekee, na kumbukumbu za malipo zinahifadhiwa na mzazi.

MCHANGANUO WA ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA ZA SHULE

1.0 Wanafunzi wanaotumia huduma zote za shule

1.1 Muhula wa kwanza

Na.	Huduma	Kipindi	Kiasi (TSH)
1	Usafiri	Muhula mmoja (miezi 6)	210,000
2	Chakula	Muhula mmoja (miezi 6)	182,000
3	Ada ya shule	Muhula mmoja (miezi 6)	180,000
4	Sare ya shule	Mwaka mzima	70,000
5	Vifaa vya shule (Stationary)	Muhula mmoja (miezi 6)	17,600
6	Huduma ya kwanza (first aid)	Muhula mmoja (miezi 6)	15,000
7	Mahafali (graduation)	Mara moja kwa mwaka	30,000
8	Mitihani (mid term and first term)	Muhula mmoja (miezi 6)	54,000
9	Safari ya shule	Muhula mmoja	25,000
10	Vifurushi vya masomo ya nyumbani (Home packages)	Muhula mmoja	14,400
Jumla ya malipo ya muhula wa kwanza			798,000

Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo ya muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026

1.2 Muhula wa pili

Na.	Huduma	Kipindi	Kiasi (TSH)
1	Usafiri	Muhula mmoja (miezi 6)	210,000
2	Chakula	Muhula mmoja (miezi 6)	182,000
3	Ada ya shule	Muhula mmoja (miezi 6)	180,000
4	Vifaa vya shule (Stationary)	Muhula mmoja (miezi 6)	17,600
5	Huduma ya kwanza (first aid)	Muhula mmoja (miezi 6)	15,000
6	Mitihani ((mid term and second term)	Muhula mmoja (miezi 6)	54,000
7	Safari ya shule	Muhula mmoja	25,000
8	Vifurushi vya masomo ya nyumbani	Muhula mmoja	14,400
Jumla ya malipo ya muhula wa pili			698,000

Tarehe ya mwisho kufanya malipo ya muhula wa pili ni tarehe 25/06/2026

1.3 Muhtasari wa malipo ya mwaka mzima

Muhula wa kwanza	Muhula wa pili	Jumla ya malipo ya mwaka
TSh 798,000	TSh 698,000	TSh 1,496,000

2.1 Wanafunzi wanaolipia ada tu

Muhula	Muda	Kiasi (TSh)
Muhula wa kwanza	Miezi sita (6)	406,000
Muhula wa pili	Miezi sita (6)	306,000
Jumla ya malipo ya mwaka	Miezi kumi na mbili (12)	712,000

Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo kwa muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026 na muhula wa pili ni 25/06/2027.

2.1 Wanafunzi wanaolipia ada na usafiri

Muhula	Muda	Kiasi (TSh)
Muhula wa kwanza	Miezi sita (6)	616,000
Muhula wa pili	Miezi sita (6)	516,000
Jumla ya malipo ya mwaka	Miezi kumi na mbili (12)	1,132,000

Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo kwa muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026 na muhula wa pili ni 25/06/2027.

2.2 Wanafunzi wanaolipia ada na chakula

Muhula	Muda	Kiasi (TSh)
Muhula wa kwanza	Miezi sita (6)	588,000
Muhula wa pili	Miezi sita (6)	488,000
Jumla ya malipo ya mwaka	Miezi kumi na mbili (12)	1,076,000

Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo kwa muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026 na muhula wa pili ni 25/06/2027.